

HEROES COMMUNITY ACADEMY (HCA)**TAARIFA NA MASHARTI YA UDAHILI WA WANAFUNZI****Ngazi ya awali (baby class day care) Mwaka****wa Masomo 2026/2027**

Heroes Community Academy ni shule ya kisasa inayotoa elimu bora kwa viwango vya juu kwa kuunganisha taaluma, maadili mema, ubunifu na maendeleo ya mtoto kwa ujumla. Dhamira yetu ni kuwajengea watoto maarifa, stadi na maadili yatakayowawezesha kuwa viongozi, wabunifu na raia wenye uwezo wa kushindana kitaifa na kimataifa.

Kwa nini uchague Heroes Community Academy?

1. Shule ina mazingira salama, rafiki na vifaa vya kisasa vya kujifunzia.
2. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika ufundishaji na mawasiliano, pamoja na programu maalumu za kuimarisha Kiingereza kwa kila darasa.
3. Walimu wenye sifa na uzoefu kutoka ndani na nje ya Tanzania.
4. Mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA/ICT).
5. Fursa za msaada wa masomo kwa baadhi ya watoto wenye changamoto za kiuchumi kupitia wadau na wafadhili wa shule.
6. Michezo na shughuli za kukuza vipaji, ubunifu na kujiamini kwa wanafunzi.

Masharti ya kujiunga na masomo

1. Mwanafunzi anayeomba kujiunga na darasa la baby class anatakiwa awe na umri kuanzia miezi sita (06) hadi miaka mitatu na nusu.
2. Mzazi au mlezi anatakiwa kuwasilisha nakala za nyaraka zifuatazo:
 - (a) Cheti cha kuzaliwa.
 - (b) Cheti cha group la damu ya mtoto anaesajiliwa (blood group type).
 - (c) Picha moja itakuwa ikiwa ni ya passport size.
3. Mzazi au mlezi anatakiwa kuwasilisha ratiba ya chakula anachotumia mtoto husika.

Masharti ya malipo kwa Mwaka wa Masomo 2026/2027

Mzazi, mlezi au mdhamini anatakiwa kusoma na kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Mdhamini, mzazi au mlezi anawajibika kufanya malipo yote ya mtoto wake kwa mujibu wa makubaliano na utaratibu uliowekwa na shule.
2. Ada ya awamu husika inapaswa kulipwa kikamilifu kabla ya mwanafunzi kuanza awamu hiyo (awamu ya kwanza na awamu ya pili)
3. Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.
4. Mdhamini, mzazi au mlezi anaweza kulipa ada za awamu zote mbili kwa pamoja.
5. Malipo yote yafanywe kupitia akaunti ya shule katika Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), kwa kutumia Control Number atakayopatiwa katika ofisi yetu.
6. Mzazi au mlezi anakubali kuwa malezi ya mtoto yanaweza kusimamishwa endapo masharti ya malipo yaliyotajwa hapo juu hayajatekelezwa ipasavyo.

Muhimu: Malipo yafanywe kwa njia zilizoidhinishwa na shule pekee, na kumbukumbu za malipo zihifadhiwe na mzazi baada ya malipo.

MCHANGANUO WA ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA ZA SHULE

1.0 Wanafunzi wanaotumia huduma zote za shule

1.1 Muhula wa kwanza

Na.	Huduma	Kipindi	Kiasi (TSH)
1	Usafiri	Muhula mmoja (miezi 6)	150,000
2	Chakula	Muhula mmoja (miezi 6)	50,000
3	Ada ya shule	Muhula mmoja (miezi 6)	150,000
4	Sare ya shule	Mwaka mzima	30,000
5	Vifaa vya kuchezea na kusomea	Mwaka mzima	50,000
6	Huduma ya kwanza (first aid)	Mwaka mzima	15,000
7	Pampas	Muhula mmoja (miezi 6)	64,000
Jumla ya malipo ya awamu ya kwanza			509,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.

1.2 Muhula wa pili

Na.	Huduma	Kipindi	Kiasi (TSH)
1	Usafiri	Muhula mmoja (miezi 6)	150,000
2	Chakula	Muhula mmoja (miezi 6)	50,000
3	Ada ya shule	Muhula mmoja (miezi 6)	150,000
4	Pampas	Muhula mmoja (miezi 6)	64,000
Jumla ya malipo ya awamu ya kwanza			414,000

1.3 Muhtasari wa malipo ya mwaka mzima

Awamu wa kwanza	Awamu wa pili	Jumla ya malipo ya mwaka
TSh 509,000	TSh 414,000	TSh 923,000

2 Wanafunzi wanaolipia ada na chakula

Awamu	Muda	Kiasi (TSh)
Awamu ya kwanza	Miezi sita (6)	359,000
Awamu ya pili	Miezi sita (6)	264,000
Jumla ya malipo ya mwaka	Miezi kumi na mbili (12)	623,000

Tarehe ya mwisho ya kufanya malipo kwa muhula wa kwanza ni tarehe 31/11/2026 na muhula wa pili ni 25/06/2027.